**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 8, Issue 1, 2025**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

*Stephen Muyundo Ndinyo[1*], Prof. Ernest Sangai Mohochi, PhD[1] na Dkt. Joseph Juma Musungu, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kibabii, S. L. P 1699-50200, Bungoma, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: muyundos@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Mei 2025*

**Istilahi Muhimu**:

*Mandhari, Mapambano, Nyimbo za kizazi Kipya, Mtandaoni na Dawa za Kulevya.*

**IKISIRI**

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni miongoni mwa masuala yanayosawiriwa katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Katika kufanya hivyo, nyimbo hizo hutumia vipengele mbalimbali vya kisanii. Mojawapo kati ya vipengele hivyo ni mandhari, huku usukaji mzuri wa mandhari ukichangia fanaka katika uwasilishaji wa ujumbe wa nyimbo hizo. Makala haya yalichunguza mandhari katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Makala yaliongozwa na Nadharia ya Utendaji katika Fasihi Simulizi iliyoasisiwa na Wallace Bacon katika mwaka wa 1957. Muundo wa kithamano mkabala wa kiutendaji ulitumika katika makala haya. Uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kukusanya data kutoka kwa video za nyimbo za kizazi kipya kuhusu dawa za kulevya katika mtandao wa YouTube ambao uliteuliwa kimaksudi. Aidha, nyimbo ziliteuliwa kimaksudi. Kisha, nyimbo hizo zilitabakishwa kidhima na kwa kurejelea aina tofauti za dawa za kulevya zinazosawiriwa. Jumla ya nyimbo 5 zilitumika. Data iliwasilishwa kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi na mijadala, mifano na dondoo kutoka kwenye uchanganuzi wa yaliyomo. Matokeo yalionyesha kwamba aina mbalimbali ya mandhari yalibainika katika video za nyimbo za kizazi kipya kuhusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni. Mandhari ya klabu, nyumbani, barabarani, mjini, mtaani na yale ya wakati yalitumika katika vita dhidi ya uraibu wa dawa za kulevya katika jamii. Aina hizi za mandhari zilotoa mchango katika kuwasilisha ujumbe kuhusu vita dhidi ya dawa za kulevya. Utafiti unapendekeza kwamba kuna haja ya kuchunguza mandhari kuhusiana na mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kurejelea aina nyinginezo za nyimbo mbali na zile za kizazi kipya. Pili, ni vyema mandhari yatafitiwe katika tanzu nyingine za fasihi pepe kama vile vichekesho, filamu na vipindi vya runinga kwa kurejelea suala la dawa za kulevya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Ndinyo, S. M., Mohochi, E. S. & Musungu, J. J. (2025). Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(1), 314-326. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

**CHICAGO CITATION**

Ndinyo, Stephen Muyundo, Ernest Sangai Mohochi and Joseph Juma Musungu. 2025. "Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (1), 314-326. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

**HARVARD CITATION**

Ndinyo, S. M., Mohochi, E. S. & Musungu, J. J. (2025) "Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), pp. 314-326. doi: 10.37284/jammk.8.1.2983

**IEEE CITATION**

S. M., Ndinyo, E. S., Mohochi & J. J., Musungu "Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya", *EAJSS*, vol. 8, no. 1, pp. 314-326, May. 2025.

**MLA CITATION**

Ndinyo, Stephen Muyundo, Ernest Sangai Mohochi & Joseph Juma Musungu. "Mandhari katika Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni Zinazohusu Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 1, May. 2025, pp. 314-326, doi:10.37284/jammk.8.1.2983.

## UTANGULIZI

Mandhari ni sehemu, mahali, eneo au hata hali ambapo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itakapotendeka (Muia, 2023). Mandhari ni kama elementi ambayo humfichulia msomaji ni wapi na lini matukio fulani yalifanyika (Wamitila, 2008). Mandhari katika nyimbo za kizazi kipya yalirejelea sehemu na hali mbalimbali zilizotumika katika kusawiri mapambano ya dawa za kulevya katika video za nyimbo za kizazi kipya. Mandhari katika nyimbo za kizazi kipya yalikuwa na nafasi kubwa katika kusawiri sifa tofauti za wahusika, maudhui mbalimbali na kuafikia lengo la waimbaji.

Dawa za kulevya ni kitu chochote ambacho huharibu fahamu au kuathiri mwili baada ya kukitumia na kumfanya mtumiaji kudhoofika kiakili (Nyamemba, 2015). Wanadamu wanashirikisha matumizi ya dawa za kulevya kama vile; bangi, mandras, heroini, kokaini, pombe za kienyeji kama chang'aa ambayo haijaruhusiwa na zilizoruhusiwa kama vile miraa, sigara na pombe (Mbeere, 2022). Dawa hizi zilikuwa na athari za kiafya kama vile uraibu, matatizo ya afya, matatizo ya kiakili, maambukizi ya Ukimwi, saratani inayohusiana na homa ya ini na uharibifu wa maini, matumizi ya dawa kupita kiasi na vifo vya mapema (Report W. D., 2022). Athari hizi miongoni mwa nyinginezo zikiwa mwiba katika jamii katika karne hii ya ishirini na moja hivyo kuangaziwa katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Makala haya yaliangazia jinsi video za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni zilichangia katika vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Mandhari tofauti yaliyokuzwa na waimbaji katika video zao za kizazi kipya yalijadiliwa kwa kina na kuonyesha yalivyochangia katika kuendeleza mapambano dhidi ya kutumiwa kwa dawa za kulevya katika jamii. Kazi hii imegawika katika sehemu sita kuu. Sehemu ya kwanza ni ile ya utangulizi, katika sehemu ya pili mjadala kuhusu mandhari katika kazi za fasihi umewasilishwa. Sehemu ya tatu imehusu nadharia ya utafiti huku sehemu ya nne ikiwa ni mbinu za utafiti. Sehemu ya tano imewasilisha matokeo ya utafiti na hatimaye sehemu ya mwisho ikitoa hitimisho la makala.

## MANDHARI KATIKA KAZI ZA FASIHI

Mandhari katika kazi za fasihi ni muhimu sana katika kuafikiwa kwa lengo la msanii kwa hadhira yake. Mandhari yana nafasi kubwa katika kukuza vipengele tofauti vya fasihi kama vile sifa za wahusika, maudhui, falsafa na lengo la kazi ile ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

fasihi. Hali hii imepelekea kutafitiwa kwa kipengele hiki cha mandhari na wasomi tofauti wa fasihi katika tanzu kadhaa kama vile hadithi fupi, ushairi na nyinginezo. Mandhari tofauti yamerejelewa na wasomi mbalimbali katika jamii kama vile mandhari ya klabuni, barabarani, nyumbani, chuoni na mtaani.

Sikuomba na Bulaya (2023) walirejelea mandhari ya kifasihi simulizi katika ujenzi wa dhamira za Ushairi Andishi kutoka katika diwani zake Muhammed Seif Khaatib. Kazi hii ililenga dhamira katika diwani za *Fungate ya Uhuru*, *Wasakaonge* na ile ya *Vifaru Weusi.* Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa mandhari yanaibua dhamira kama vile kutokuheshimu taaluma, uzalendo wa kweli, ukombozi wa kifikra, ujasiri na ukombozi. Kwa hiyo, mandhari ya kifasihi simulizi yalitumika kuibua dhamira ambazo zinaakisi uhalisia wa maisha halisi ya tabaka tawala na tawaliwa katika jamii. Kazi hii iliweka msingi dhabiti wa kuangalia msingi wa dhamira za waimbaji wa wasanii wa nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mutisya (2021) naye aliangazia usawiri wa mandhari katika riwaya za *Embe Tamu*, *Siku ya Wajinga* na *Njiapanda*. Utafiti huu ulibainisha mandhari tofauti katika kazi tatu teule kama ifuatavyo; Katika *Embe Tamu* mandhari ya ghala, sokoni, usafiri, ufugaji na ya mvua yamesawiriwa. Aidha, mandhari ya ukuaji wa mimea, uharibifu wa mazingira na mjini. Vile vile, katika *Siku ya Wajinga*, mandhari ya nyumbani, shuleni, darasani, michezoni, makaburini na hospitalini. Hatimaye katika *Njiapanda*, mwandishi amesawiri mandhari ya barabarani, kidhahania, shuleni na hospitalini. Kazi hii italenga kubainisha iwapo mandhari haya pia yalijitokeza katika mapambano ya dawa za kulevya katika video za nyimbo za kizazi kipya.

Mavisi na Wendo (2022) walishughulikia usawiri wa mandhari kibibliotherapia katika hadithi fupi teule za Kiswahili**.** Wasomi hawa walidhihirisha kwamba bibliotherapia hujitokeza katika mandhari yanayosawiriwa katika diwani hizi za hadithi fupi: *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Mandhari yalibainika katika hali halisi ya maisha ya wanafunzi wa shule za upili. Mandhari ya shuleni, nyumbani, mashambani na mjini yalisawiri hali halisi katika maisha ya wanafunzi. Matokeo kuhusu mandhari katika hadithi fupi teule yalionyesha umuhimu wake katika kuathiri tabia ya mwanafunzi. Hata hivyo, mandhari ya sehemu za vilabuni na danguroni kama vile katika hadithi za *Nipe Nikupe*, *Samaki wa Nchi za Joto na Gilasi ya Mwisho Makaburini* huenda zisitimize bibliotherapia kwa wanafunzi. Utafiti huu ulilenga kubainisha hali hii inavyojitokeza katika nyimbo za kizazi kipya hususan kwa kurejelea vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii.

Muia (2023) alichunguza mchango wa mandhari katika kufanikisha ujumbe wa waandishi wa riwaya za *Maisha Kitendawili* na *Rosa Mistika*. Utafiti huu uligundua kuwa mandhari ni muhimu sana kwa waandishi kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Kwanza ilibainika kuwa mandhari ya aina mbalimbali yalitumiwa na waandishi hawa. Mandhari haya yalikuwa ni mandhari ya mahali, mandhari ya wakati na mandhari ya hali. Pili, msomi huyu alipata kuwa ujumbe unaofanikishwa na mandhari hayo ulikuwa ni utabaka, dhuluma zinazodhihirika katika jamii za waandishi, uvumilivu katika ndoa, utamaduni na nafasi ya mwanamke. Hatimaye, waandishi walitumia mandhari halisi ambayo yanadhihirika katika jamii zetu. Masuala haya ya ndoa, utamaduni na nafasi ya mwanamke yalibainika moja kwa moja katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Mandhari ya baa yalikuwa sehemu ya kucheza dansi, kunywa pombe, Rosa kukutana na Deogratius na mahusiano ya kimapenzi kuanza kati yao, kulewa ili kusahau misiba iliyowafika na kujifurahisha (Muia, 2023). Pia ujanja wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

wanawake na ujinga wa wanaume na unyonyaji wa wanaume ulijitokeza. Kisha baa ilitumika kuonyesha uozo katika jamii kama vijana kulewa wakiwa kwa umri mdogo, kutapeliwa na kuibiwa kwa watu wakiwa walevi. Hali hizi vile vile zilibainika moja kwa moja katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni.

Gitau, Mutai na Gitonga (2016) katika kuchunguza kuhusu masuala yanayohusiana na kanuni za uuzaji wa pombe katika manispaa ya Thika Kaunti ya Kiambu, waligundua kwamba mandhari ya madongoporomoka yalichangia unywaji wa pombe kwa wakaaji wao kutokana na changamoto zao za kijamii na kiuchumi. Suala hili la unywaji wa pombe katika eneo la madongoporomoka lilibainika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni.

Hali ya maisha ya Barabara ya Koinange wakati wa usiku inaangaziwa na Mavisi na mwenzake (2022) ambao wanadhihirisha kuwa mandhari ya usiku yalichangia ubakaji na kupata ujauzito na ukahaba. Pia mandhari haya yamefichua dhuluma za wana jamii mikononi mwa polisi na hali za gereza na mazingira duni ya korokoroni. Mandahari haya ya usiku yalibainisha athari za uraibu wa dawa za kulevya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

## NADHARIA YA UTAFITI

Nadharia ya Utendaji katika Fasihi Simulizi iliasisiwa naye Wallace Bacon katika mwaka wa 1957. Ndiyo iliuongozo utafiti huu. Nadharia hii inahusishwa na kazi zao Turner (1988) na Schechner (1985). Wasomi hawa wawili walirejelea asili ya utendaji kwa jamii kote ulimwenguni, vile matukio na matambiko katika maisha yetu ya kila siku yaliongozwa na kanuni za utendaji. Nadharia hii ya Utendaji wa fasihi simulizi inashikilia kwamba kila mmoja wetu hushiriki katika utendaji katika jamii. Hii ni kupitia kwa mavazi yetu, mazungumuzo yetu au chakula tunachokula, yote haya yameundwa kama mfumo wa ishara kwetu wenyewe na kwa wengine katika jamii kuhusu nafasi yetu katika makundi yetu ya kijamii.

Nadharia hii ina mihimili sita (6) kama ifuatavyo (Foley, 2002); Kwanza, utendaji wa fasihi simulizi una kodi maalum kama vile lahaja na mavazi mahususi. Pili, lugha ya kitamathali kama vile tashbihi, jazanda na nahau miongoni mwa tamathali nyinginezo za semi hutumika. Tatu, utendaji wa fasihi simulizi huwa na usambamba kwa kuwepo kwa aya zinazojitegemea kimuundo na kufanya kazi kwa pamoja. Nne, fomula maalum hujitokeza katika utendaji wa fasihi simulizi kama vile misemo inayorudiwa na sarufi. Tano, kigezo cha mila na utamaduni kinachoshikilia kwamba tanzu za fasihi simulizi husalia vivyo hivyo licha ya kubadilika kwa ulimwengu. Hatimaye, sita ni kuwa upekee wa utendaji katika fasihi simulizi unaojitokeza kwa nyimbo za kutanguliza na mwito mbalimbali.

Kazi hii iliongozwa na mhimili mmoja (1) kati ya ile sita (6). Mhimili wa sita wa nadharia hii unaoshikilia kwamba upekee wa utendaji katika fasihi simulizi unaojitokeza kwa nyimbo za kutanguliza na mwito mbalimbali ndio uliotumika katika uchunguzi huu. Mandhari yalikuwa mojawapo ya vipengele vya upekee wa utendaji. Mandhari yalikuwa ni nguzo muhimu katika upekee wa video yeyote ile ya nyimbo za kizazi kipya. Mandhari yalikuwa na nafasi kubwa katika kusawiri mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika video. Kwa hivyo madhari tofauti yalitumiwa kwa njia tofauti na waimbaji katika kuafikia malengo yao ya kuwasilisha ujumbe wa kupinga uraibu wa dawa za kulevya katika video za miziki ya kizazi kipya. Mjadala kuhusu nafasi ya mandhari katika nyimbo za kizazi kipya zinazohusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya ulijikita katika upekee wa kiutendaji unaoendana na mandhari mbalimbali katika kazi hizo.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala haya yalitumia muundo wa kithamano mkabala wa kiutendaji. Mkabala wa kiutendaji ni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

uchunguzi wa kitaratibu unaolenga kupata suluhu mwafaka kwa matatizo wanayokumbana nayo wana jamii kila siku (Stringer, 2007). Muundo huu wa kiutendaji hulenga suala ibuka ambalo huhitaji suluhu la moja kwa moja dawa za kulevya katika jamii ikiwa mojawapo.

Makala haya yalilenga kushirikisha nyimbo za kizazi kipya za Kiswahili. Nyimbo zilizochaguliwa ni zile za kizazi kipya hususan zilizorejelea suala ibuka la dawa za kulevya. Mtandao wa *YouTube* ulilengwa katika utafiti huu kama jukwaa la kupakua na kuchezwa kwa nyimbo mbalimbali zikiwemo za kizazi kipya.

Mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi ilitumika katika kuchagua nyimbo za kizazi kipya za Kiswahili, nyimbo zilizolenga suala ibuka la dawa za kulevya na na mtandao wa *You Tube*. Usampulishaji wa kitabaka ulitumika katika kugawa nyimbo za kizazi kipya katika matabaka kidhima kwa kusawiri suala la dawa za kulevya. Pia nyimbo ziliwekwa kwa matabaka tofauti kwa kurejelea madawa ya kulevya yaliyojitokeza katika nyimbo hizo. Jumla ya nyimbo tano (5) zilishirikshwa katika utafiti huu.

## UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

Data iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa njia ya kithamano. Mkabala huu ulikuwa mwafaka katika kazi hii kwa vile ulieleza vipi na kwa nini matukio yalitokea (Kress, 2008). Jwan & Ong'ondo (2011) anaeleza kwamba mchakato wa uchanganuzi data ulifuata hatua sita kuu. Kwanza mtafiti alinakili kwenye mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo data muhimu aliyosikiliza na kutazama katika video za muziki katika mtandao wa *YouTube*. Mtafiti alirudia kusoma data aliyoandika huku akirudia mchakato wa kutazama na kuzikiliza nyimbo zile za kizazi kipya teule hadi alipofikia sampuli dabwadabwa.

Kisha, data iliyonakiliwa ilisomwa ili kupata maana ya jumla kuhusiana na mandhari katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Hii ilisaidia kutambua aina tofauti za mandhari zilivyojitokeza katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Vile vile, hatua ya usimbaji wa data iliyokusanywa kuhusu mandhari katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni ulifanywa. Mtafiti alitumia usimbaji kubainisha mandhari mbalimbali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni kwa kurejelea upya data iliyonakiliwa.

Aidha, data ilichanganuliwa kwa kujikita kwa mmandhari yalivyotumika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtndaoni katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Mifano ya mandhari mbalimbali kutoka katika data kuhusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni ilichanganuliwa.

Mkabala wa kithamano ulikuwa mwafaka kwa utafiti huu kwa vile kulikuwa na data zilizoelezwa kwa njia ya kimaelezo kuelezea mandhari mbalimbali yaliyobainika. Uchanganuzi na wa data iliyokusanywa ulifanywa kwa utaratibu kwa kuongozwa na nadharia ya Utendaji katika Fasihi Simulizi. Mandhari mbalimbali yalidhihirika moja kwa moja katika video za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Mandhari ya klabuni, nyumbani, barabarani, mjini, mtaani na wakati yalichanganuliwa na kuhakikiwa kwa kina kwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Hatimaye, matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kifafanuzi katika aya na dondoo kutoka kwa mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo wa sehemu muhimu za nyimbo teule. Vile vile, mijadala iliibuliwa kutokana na matokeo ya utafiti na ufafanuzi wa kina wa data kufanywa. Hatimaye, kulikuwepo na hitimisho na mapendekezo kutokana na matokeo aliyopata katika kazi hii.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

## UHALALI NA UTHABITI WA VIFAA

Uhalali wa kifaa ni kipimo anachotumia mtafiti kuhakikisha kuwa kuna ufaafu na utendakazi wa kifaa husika (Kombo & Tromp, 2006). Kifaa cha mwongozo wa yaliyomo ndicho kilichotumika katika utafiti huu kukusanya data. Mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumiwa kupata data kutoka kwa nyimbo mbili (2) teule za kizazi kipya mtandaoni. Nyimbo hizi mbili teule zilikuwa ni wimbo wa *Gin ama Whiskey* wao Breeder LW pamoja na Mejja na ule wa *Lenga* wao Willy Paul akishirikiana na Size 8 Reborn. Majaribio haya yalimwezesha mtafiti kuhakikisha mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo ni faafu katika utendakazi wake kwake. Utafiti mwigo ulifanywa ili kupata data kuhusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni katika nyimbo za kizazi kipya. Hili lilimwezesha mtafiti kupata habari sahihi zilizohitajika kutimiza malengo ya utafiti huu.

Uthabiti ni kiwango ambacho kifaa cha utafiti kinaweza kutoa matokeo yaliyo sawa baada ya majaribio kadhaa. Mtafiti kupitia kwa utafiti wa hapo mbeleni alihakikisha kwamba matokeo ya utafiti yalitoa habari sawa. Hii ilifanyika kwa mtafiti kutumia uchanganuzi wa yaliyomo wa nyimbo mbili (2) teule mtandaoni. Data aliyokusanya mtafiti ilimwezesha kuhakikisha kuwa matokeo aliyopata hatimaye hayakubadilika baada ya majaribio na marekebisho mara nne (4). Mtafiti alikifanyia marekebisho kifaa cha uchanganuzi wa yaliyomo kwa kuongeza vigezo zaidi vya kuangaziwa, kujitokeza kwa vipengele muhimu na kukielewa kifaa cha utafiti. Kifaa hiki kilipitiwa na wasimamizi wa utafiti na kikachongwa zaidi kabla ya matumizi yake.

## MAADILI YA KITAFITI

Maadili ya utafiti ni nguzo muhimu katika utafiti wowote ule. Burns (2000), Kristin (2002) na Ogechi (2024) wanapendekeza maadili yafuatayo yaliyoongoza utafiti huu. Mtafiti alianza kwa kuzingatia sheria na sera za kitaasisi na kiserikali kwa kutafuta kibali kutoka kwa Shule ya Shahada za Juu katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Baada ya kupata kibali hicho, mtafiti alitafuta idhini ya dola kwa kutafuta kibali kutoka kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Baraza la Sayansi, Teknolojia na uvumbuzi (NACOSTI) katika Wizara ya Elimu.

Mtafiti pia alizingatia uyakinisho na alipunguza au kukoma kabisa kudhihirisha upendeleo. Kisha, mtafiti alihakikisha kuwa data alizokusanya za nyimbo za kizazi kipya na matokeo ya utafiti huu yalihifadhiwa kwa siri. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yalitumika tu kwa minajili ya utafiti uliokusudiwa wala sio kwa sababu zingine zozote zile. Mwishowe, kazi za wataalam wengine zilitambuliwa kwa kunukuliwa kwenye makala na kujumishwa katika marejeleo ili kuepuka wizi wa kitaaluma.

## MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA

Mandhari yalikuwa ni mojawapo ya kipengele muhimu katika video zote za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Mojawapo ya uamilifu wa mandhari ikiwa ni ujenzi wa upekee wa video husika ya kizazi kipya na lengo la kuwavutia watazamaji wengi. Vile vile, mandhari yalipaswa kuhakikisha kwamba ujumbe wa mwimbaji ulipokelewa moja kwa moja. Makala haya yalibainisha mandhari tofauti katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mandhari ya klabu, mandhari nyumbani, mandhari ya barabarani, mandhari ya mjini, mandhari ya mtaani na mandahri ya wakati yalijadiliwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kupitia video za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

### Mandhari ya Klabu katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya

Klabu huwa ni maeneo yaliyotengewa kwa kujiburudisha katika jamii ya kisasa. Mandhari haya yalikuwa sehemu ya kucheza dansi, kunywa pombe, watu kukutana na mahusiano ya kimapenzi kuanza kati yao, kulewa ili kusahau misiba iliyowafika na kujifurahisha (Muia, 2023). Video za nyimbo za kizazi kipya zilisawiri mandhari haya ya klabu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

kama maeneo ambayo wana jamii huburudika kwa njia tofauti kama vile kusikiliza muziki, kucheza dansi, kutulia na kujiliwaza huku wengine wao wakijihusisha katika uraibu wa dawa za kulevya. Mojawapo ya njia ya kujistarehesha ikiwa ni matumizi ya dawa mbalimbali za kulevya. Wimbo mmoja (1) wa kizazi kipya ulirejelea klabu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Wimbo huu ulikuwa ule wa *Pombe* wake Rose Muhando. Wimbo huu ulisawiri mandhari ya klabu kwenye video yake ya kizazi kipya katika kupinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Matumizi ya dawa za kulevya yalibainika moja kwa moja katika wimbo wa kizazi kipya wa *Pombe* wake mwimbaji Rose Muhando. Kwanza wimbo huu unapinga unywaji wa pombe katika video yake. Kijana anaonekana akinywa bia pamoja na vipusa wawili wanaokunywa mvinyo. Kijana huyu analewa chakari kutokana na unywaji wa kupindukia wa bia kumi na vipusa wale wanamuibia kibeti na stakabadhi zake za kazi.

Rose Muhando pia anasawiri matumizi ya dawa haramu katika klabu. Uvutaji wa bangi kwenye klabu ulidhihirika kupitia kwa mama bonge wawili pamoja na mwanamume mmoja wa makamo. Mandhari haya yanaonyesha kuwa licha ya bangi kuwa ni mojawapo ya dawa haramu, kulikuwepo na baadhi ya vilabu vilivyoiuza na kuvutwa hadharani. Vile vile, ilibainika wazi kuwa unywaji wa pombe katika klabu huandamana pamoja na matumizi ya dawa nyinginezo kama bangi katika jamii.

Mapenzi bandia yaliweza kudhihirika moja kwa moja kutokana na mandhari ya klabu katika wimbo wa *Pombe* wake Rose Muhando. Wasichana hawa warembo wanatumia uvutaji huu kwa kuvuta na kumpulizia mwanamume yule mdomoni. Uvutaji huu unatumika kuashiria mapenzi ya bandia kwa vile ni njia ya kumsisimua kimapenzi ili wafanikishe njama yao ya kumuibia. Baadaye mwanamume huyu wa makamo anatimuliwa na vijana akiwa chumbani na mmoja wa mama bonge wale.

Hatimaye mandhari ya klabu yalisawiriwa kama pahali pa kucheza densi katika jamii. Wimbo huu unamsawiri mama bonge akicheza densi huku akivuta bangi mbele ya mwanamume wa makamo aliyeketi akinywa pombe. Kucheza densi kwake mama bonge kulinuia kumtongoza mwanamume yule katika klabu. Mama bonge yule, katika kucheza mbele yake mwanamume yule huku akimtingizia makalio yake, alinuia kumsisimua kimapenzi. Mwishowe inajitokeza wazi kuwa mwanamume yule analaghaiwa na kupelekwa chumbani na mama bonge yule kabla ya kutimuliwa na vijana.

Hivyo basi, mandhari ya klabu yanafanikisha lengo lake la kuwatahadharisha wana jamii dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Wimbo huu ulibainisha wazi kutoka kwa mandhari ya klabu kwamba matumizi ya dawa za kulevya yalikuwa na athari katika jamii. Mandhari haya yalipaswa kuwabainishia wana jamii maovu yanayowafika walevi katika klabu ili waepukane na matumizi ya dawa za kulevya tofauti katika klabu.

**Mandhari ya Nyumbani katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya**

Nyumbani huwa ni sehemu moja tulivu na yenye amani katika jamii yeyote ile na hupaswa kuwa na mazingira salama kwa familia yoyote ile. Wimbo wa kizazi kipya wa *Pombe* wake Rose Muhando ulisawiri vita dhidi ya dawa za kulevya nyumbani katika jamii ya kisasa. Mapambano haya dhidi ya dawa za kulevya katika mandhari ya nyumbani yanabainika kama inavyoelezwa hapa.

Kwanza wimbo wa *Pombe* wake Rose Muhando ulipinga matumizi ya dawa za kulevya kwa kurejelea mandhari ya nyumbani. Wimbo huu unawasawiri wanafunzi wawili wakiwa wamevalia sare za shule na wameketi mlangoni na bahasha ya salio la karo mkononi. Wanafunzi hawa wametimuliwa shuleni kwa kutolipa karo yao. Baba yao anapowasili ni mlevi chakari akiwa na kopo la pombe mkononi na punde tu anapokabidhiwa karatasi ya salio la karo anaanguka na kulala

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

kifudifudi na kupoteza fahamu. Mandhari haya yalisawiri athari ya pombe nyumbani haswa kwa kuathiri elimu ya watoto katika jamii. Wimbo huu ulionyesha kutolipwa kwa karo kama mojawapo ya athari ya matumizi ya kupindukia ya dawa za kulevya. Hivyo wimbo huu unalenga kuhamasisha jamii kuepukana na uraibu wa dawa za kulevya ili tuwajibikie majukumu yetu.

Kisha kutelekeza familia pia kulijitokeza katika mandhari ya nyumbani. Mandhari ya nyumbani yalimsawiri mwenye nyumba akija kufunga nyumba, huku rai zake mama na watoto kutofungiwa kwa nyumba ile zikiambulia patupu. Hali hii ilitokana na baba kupotelea ulevini huku kodi ya nyumba ikiwa haijalipwa. Mandhari haya ya nyumbani yamesawiri jinsi familia zinaathirika kutokana na uraibu wa dawa za kulevya. Uraibu huu unaipokonya familia haki za kimsingi kama vile elimu na makazi kwa baba kutokomea kwa ulevi. Manthari haya yalilenga kudhihirisha moja kwa moja kwamba familia iliathirika kutokana na uraibu wa dawa za kulevya. Mandhari haya yalilenga kuhamasisha jamii dhidi ya uraibu wa dawa za kulevya ili wawajibikie familia zao.

Hivyo basi, mandhari haya ya nyumbani yamechangia katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika jamii. Kusawiriwa kwa kuteseka kwa familia pale nyumbani kwa baba kutelekeza majukumu yake kwa sababu ya uraibu wa pombe. Lengo la video hii likiwa kuwatahadharisha wana jamii dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ili wasipoteze familia zao kwa sababu ya uraibu wa pombe. Wana jamii wanahitajika kujiepusha na uribu wa dawa za kulevya ili wawajibikie familia zao katika jamii.

**Mandhari ya Barabarani katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya**

Barabara ilijitokeza kama mandhari katika nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Jumla ya nyimbo mbili (2) za kizazi kipya zilisawiri mandhari haya ya Barabara katika video zake. Nyimbo hizi ni wimbo wa *Mihadarati* wa Simple Boy na ule wa *Pombe* wake Rose Muhando. Mandhari haya ya barabarani yalidhihirika katika video za kizazi kipya kama ifuatavyo.

Kwanza mandhari haya yalitumika kwenye video za kizazi kipya kusawiri ukosefu wa heshima katika jamii. Wimbo *Pombe* wake Rose Muhando ulimsawiri mwanamume wa umri wa makamo akionekana akianguka na kopo la pombe mkononi. Kila alipoanguka na kusimama alichekelewa na kikundi cha watoto kwa kulewa chakari. Mandhari haya yalitumika katika kuashiria kupotea kwa heshima yake katika jamii kwa kuwatumia watoto wadogo kumchekelea kwa kulewa chakari. Kitendo hiki kinatumika kijazanda kuashiria kuwa ulevi wa kupindukia husababisha ukosefu wa heshima katika jamii. Mandhari haya yalilenga kuangazia athari mojawapo ya uraibu wa dawa za kulevya ili kuwazuia wana jamii kujiingiza katika uraibu huu. Kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya kupindukia kulikuwa muhimu kwa vile wana jamii walisalia na heshima yao katika jamii.

Mandhari ya barabarani pia yalitumika katika kuangazia athari ya ulevi katika jamii. Mwanamume wa umri wa makamo anaonekana akikimbizwa mbio na vijana barobaro. Vijana hawa walikuwa wamemfumania na mama bonge kitandani na hivyo kumtimua mbio. Mandhari haya yanamwonyesha mwanamume huyu akikimbia kwa kasi huku vijana wale wakimfuata unyo unyo. Mandhari haya yaliashiria athari ya uasherati unapofumaniwa na mwanamke asiye mke wako. Hivyo mandhari haya yanalenga kututahadharisha tuepukane na dawa za kulevya ili tusijipate katika mitego kama vile usherati katika jamii.

Mwishowe wimbo *Mihadarati* wake mwimbaji Stivo Simple Boy ulisawiri mandhari ya barabarani katika video hii yake. Mwimbaji anaonekana akiimba na kucheza dansi pamoja na vijana wengine akiwa barabarani. Mandhari haya yanawashirikisha vijana katika kucheza barabarani. Mwimbaji huyu Simple Boy amekuwa mbunifu kwa kurejelea sehemu mbalimbali za barabara kama vile kando ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

barabara ipitayo juu ya nyingine, chini ya barabara hiyo na kando yake. Mandhari haya yalitumika kuashiria usasa katika wimbo huu haswa kwa kuwashirikisha vijana katika kucheza dansi. Hili lilikuwa muhimu katika kuwakomboa vijana kutoka kwa matumizi ya dawa za kulevya. Hii ni kwa sababu idadi kubwa ya vijana ndio waliojitosa katika suala hili la dawa za kulevya na ilikuwa vyema kuwashirikisha katika vita hivi dhidi ya dawa za kulevya. Pia anaonyesha kwamba vijana wanaweza kucheza popote pale dansi sio lazima iwe katika eneo la burudani kama vile katika klabu na baa wanakojitosa katika matumizi ya dawa za kulevya. Hivyo anaendeleza vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii kwa kudhihirisha kuwa vijana wanaweza kujuburidisha kwa kucheza dansi bila matumizi ya dawa za kulevya.

Mandhari ya barabarani yalikuwa na nafasi nzuri katika video za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni katika vita dhidi ya dawa za kulevya katika jamii. Mandhari haya yalisawiri athari ya uraibu wa dawa za kulevya kwa waraibu ikiwa ni kujidhahilisha katika jamii. Wana jamii walipaswa kuepukana na uraibu wa dawa za kulevya ili waheshimike. Mwishowe wimbo wa *Mihadarati* wa Stivo Simple Boy ukirejelea njia mbadala ya vijana kujiburudisha katika jamii kwa kucheza densi badala ya kutumia dawa za kulevya.

### Mandhari ya Mjini katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya

Miji ni sehemu zenye kivitio kikubwa kwa watu kutoka kwa sehemu mbalimbali kutokana na maendeleo yake. Mandhari ya mjini pia yalitumika katika video ya wimbo mmoja (1) wa kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Wimbo wa *Pombe* wake mwimbaji Rose Muhando ulisawiri mandhari ya mji wa *Nairobi* kwa kuonyesha mtaa wa *Koinange* kuliko hawara wanaowangojea wateja wao. Hawara hawa wapo gizani huku wakiwa wamevalia nguo fupi zilizowabana miili yao. Mandhari haya yalidokeza hali halisi waliyokumbana nayo waraibu wa dawa za kulevya punde tu walipolewa. Walevi hawa ndio waliokuwa windo la hawara hawa kwa kushiriki nao mapenzi kiholela na wakati wengine kuwaibia chochote walicho nacho. Wimbo huu wa Pombe ulinuia kuwatahadharisha waraibu wa dawa za kulevya kuepukana na ulevi wa kupindukia ili wasijitose katika usherati na hawara hawa katika mitaa kama ule wa *Koinange.*

Pia msanii huyu anaonyesha kibandiko cha klabu maarufu ya *Sabina Joy* ambayo imejulikana kwa usherati. Mandhari haya ya *Sabina Joy* yalirejelea sehemu ya ulevi na usherati. Wimbo huu unatumia mandhari haya kijazanda kurejelea suala sugu la mihadarati na uhusiano katika jamii. Hivyo basi, mandhari haya yanawahimiza waraibu wa dawa za kulevya kuepukana na dawa za kulevya ili kujikwamua katika mtego wa usherati kwa vile usherati na uraibu wa dawa za kulevya zinafungamana. Mandhari haya ya mjini katika video ya wimbo *Pombe* wake Rose Muhando yalisawiri suala la usherati kwa kulihusisha na dawa za kulevya. Waraibu wengi wa dawa za kulevya walilewa kwenye klabu zilizoko mjini kutokana na usasa wake. Mwishowe baada ya kulewa wakati mwingine walijihusisha kwa usherati kama inavyobainika katika mandhari ya mtaa wa *Koinange* na yale ya klabu ya *Sabina Joy.* Mandhari haya yalilenga kuwatahadharisha walevi kuepukana na dawa za kulevya ili kuepuka kujiingiza katika usherati.

### Mandhari ya Mtaani katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya

Video hizi za nyimbo za kizazi kipya zimesawiri vijana katika mitaa mbalimbali. Mitaa ilikuwa ni sehemu muhimu kwa vile ilisheheni shughuli mbalimbali za wana jamii. Mandhari ya mtaani yamesawiriwa katika video ya nyimbo mbili (2) za kizazi kipya. Nyimbo hizi ni *Mihadarati* wake Rusty Gee na ule wake Stivo Simple Boy. Mandhari haya yalitumiwa kwenye video za kizazi kipya katika kupinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Nyimbo hizi mbili za *Mihadarati* zao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

waimbaji Rusty Gee na Stivo Simple Boy zilirekodiwa kwenye mtaa wa madongoporomoka. Mitaa hii ya madongoporomoka ilitumika katika kuashiria makaazi duni kunakouzwa dawa za kulevya kwa wingi. Vile vile, mitaa hii ya madongoporomoka pia iliongoza kwa uuzaji wa dawa haramu kwa sababu ya kipato cha chini cha wakaaji wao. Kwanza wimbo wake Rusty Gee uliwahusisha watoto na vijana waliokuwa na mabango tofauti ambayo yalipinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Vijana hawa waliwakilisha wana jamii wanaoathirika na janga hili la dawa za kulevya kwa kiwango kikubwa. Mandhari haya ya mtaani yaliwahusisha kwa mapambano haya dhidi ya dawa za kulevya.

Hatimaye watoto pia walihusishwa katika kushika mabango dhidi ya dawa za kulevya katika jamii. Hii ilikuwa muhimu kwa vile wao ndio kizazi cha siku za usoni na kilihitaji kulindwa dhidi ya janga hili la dawa za kulevya. Vile vile, kuhusishwa kwa watoto katika mapambano haya ya dawa za kulevya kuliwawezesha kuepukana kushawishiwa kwa wepesi kutumia dawa mbalimbali za kulevya. Mandhari haya yalitimiza lengo la kuwahusisha watoto katika vita dhidi ya dawa za kulevya.

Maandamano ya wana jamii pia yalisawiriwa katika mandhari haya ya mtaani kwenye video za kizazi kipya. Wimbo wa *Mihadarati* wake mwimbaji Stivo Simple Boy pia ulihusisha mabango yaliyopinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Tofauti naye Rusty Gee ambaye vijana walisimama naye, msanii Stivo Simple Boy aliwahusisha vijana wakiandamana naye katika wimbo wake. Kunadamana huku katika mtaa huu kuliashiria kupitisha ujumbe kwa wana jamii kuhusu matumzi ya dawa za kulevya. Mandhari haya ya maandamano yalihusiksha vijana na watoto na mabango wakiandamana mtaani, hali iliyoashiria kushirikishwa kwa vijana na watoto katika vita dhidi ya mihadarati katika jamii.

**Mandhari ya Wakati katika Video za Nyimbo za Kizazi Kipya**

Wamitila (2003) akirejelea mandhari ya wakati, anasema kuwa dhana hii hutumika kurejelea kipindi ambacho hali na matukio yanayosimuliwa na uwasilishaji wake hutokea. Kazi hii ilirejelea mandhari ya mchana na mandhari ya usiku katika nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Vile vile, kulikuwepo na nyimbo zilizoshirikisha mandhari yote, usiku na mchana katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

***Mandhari ya Mchana katika Video za Nyimbo za kizazi Kipya***

Wakati wa mchana ni majira muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku katika jamii. Wakati wa mchana huambatana na mwanga wa jua, joto, na hali ya uwazi, na mara nyingi hutumika kuonyesha au kutoa mwelekeo wa kipekee katika kazi ya fasihi. Kwa mfano, mchana unaweza kuashiria mambo kama matumaini, shughuli au ufahamu kwa sababu ya mwangaza unaokuja na wakati huu wa siku (Baker, 2019). Wakati huu wa mchana vile vile ulijitokeza katika video za nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mandhari haya ya mchana yalisawiriwa na nyimbo tano (5) za kizazi kipya katika video zake katika vita dhidi ya suala hili ibuka la dawa za kulevya. Nyimbo hizi zilikuwa *Pombe* wake Rose Muhando, *Bangi* wa Nduati, *Mihadarati* wao Domani Mkadinali, Stivo Simple Boy na mwenzao Rusty Gee. Nyimbo nne (4) zilisheheni mandhari haya ya mchana pekee katika video zake. Nyimbo hizi zilikuwa ni wimbo *Bangi* wake Nduati, *Mihadarati* wao Domani Mkadinali, Stivo Simple Boy naye Rusty Gee. Hata hivyo, wimbo *Pombe* wake Rose Muhando ulirejelea mandhari ya wakati wa mchana na yale ya usiku.

Mandhari haya ya mchana yalikuwa ya kimsingi kwa vile yalisheheni baadhi ya mandhari mengineyo. Kwanza mandhari ya mchana yalitumika kuonyesha athari ya dawa za kulevya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

katika jamii. Wimbo wa Pombe wa mwimbaji Muhando ulionyesha athari ya dawa za kulevya wakati wa mchana. Mandhari haya yalionyesha kwamba unywaji wa pombe haramu ulisababisha waraibu wake kulala mtaroni na kopo la pombe kando yake kwa kulewa chakari na ugomvi miongoni mwa walevi katika kibanda chake mama pima.

Mandhari ya mchana pia yalitumika kusawiri athari ya matumizi ya dawa za kulevya katika familia. Kwanza wanafunzi wawili wameketi mlangoni baada ya kufukuzwa shuleni kwa sababu ya kutolipiwa karo, watoto hawa wametelekezwa na baba yao kwa kutoshughulikia mahitaji yao na kumlazimu mama kuwajibika kwa kuchuuza mboga mitaani. Pia mandhari haya ya mchana yalitumika kusawiri athari ya unywaji wa pombe kuwa mlevi kuangushwa na watoto wakimcheka kama ishara ya ukosefu wa heshima katika jamii.

Mandhari ya mchana pia huchochea hisia za uwazi wa maono, ikilinganishwa na mandhari ya usiku ambayo mara nyingi yanaonekana kuwa ya siri au ya hofu (Jones na wenzake 2021). Mandhari ya mchana vile vile yalisawiri vita dhidi ya dawa za kulevya katika jamii. Nyimbo mbili (2) za *Mihadarati* zao Stivo Simple Boy naye Rusty Gee zilihusisha maandamano dhidi ya dawa za kulevya. Mandhari haya yaliwaonyesha vijana na watoto wakiwa na mabango yenye kuhamasisha jamii dhidi ya dawa za kulevya katika jamii. Mandhari haya ya mchana yalitumika kijazanda kuonyesha kuwa vita hivi dhidi ya dawa za kulevya vilikuwa ni wazi kwa kuwa suala hili la dawa za kulevya lilikuwa ni mwiba katika jamii. Mwishowe mandhari ya mchana vile vile yalitumika kijazanda kurejelea mwangaza kwa kuwakomboa wana jamii kutokana na janga hili.

### *Mandhari ya Usiku katika Video za Nyimbo za kizazi Kipya*

Katika jamii nyingi za Kiafrika, kuna imani kwamba matendo maovu hutendeka usiku (Mavisi na mwenzake, 2022). Mandhari haya ya usiku yalijitokeza katika video ya wimbo mmoja (1) wa kizazi kipya katika. Wimbo wa *Pombe* wake mwimbaji Rose Muhando ulihusisha mandhari haya ya usiku katika kuyapinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii.

Kwanza mandhari ya usiku yalionyesha walevi wa kiume wawili katika klabu wakinywa pombe pamoja na wanawake wakati wa usiku. Mlevi wa kwanza anakunywa bia na wasichana wawili wanaokunywa mvinyo na baadaye anapolewa chakari anaibiwa kibeti na stakabathi zake katika mkoba wake. Vile vile, mwenzake pia anakunywa pombe pamoja na mama bonge wawili huku akivuta bangi na wanawake wawili katika klabu. Mlevi huyu anapangiwa njama ya kutimuliwa na vijana baada ya kuhadaiwa na kupelekwa chumbani na mwanamke mmoja.

Mandhari haya ya usiku yametumiwa katika wimbo huu wa Pombe katika kuangazia suala la usherati katika jamii. Mandhari haya yalidhihirisha wazi kuwa walevi wengi walihusisha ulevi na usherati kwa vile wote wanalewa pamoja na wanawake. Kisha mandhari haya yalionyesha maovu wanayotendewa walevi katika jamii usiku wa manane. Mwishowe, mandhari ya usiku pia yalionyesha ubakaji wa mwanamke mlevi aliyekuwa na bia mkononi. Vijana wawili wanamnyanyua na kumbaka mwanamke huyu katika maegesho ya gari punde tu anapotoka katika klabu. Wimbo huu wa *Pombe* hivyo basi ulinuia kuonyesha athari ya matumizi ya dawa za kulevya kwa waraibu wake haswa wakati wa usiku katika jamii. Mwimbaji huyu anaafikia lengo lake kwa kuonyesha athari ya matumizi ya dawa za kulevya wakati wa usiku kwa jamii.

Mandhari ya usiku katika wimbo *Pombe* wake Rose Muhando yaliangazia zaidi suala hili la usherati kwa kusawiri makahaba waliosimama katika mtaa wa *Koinange* kwa sehemu za giza wakiwa wamevalia nguo fupi na zilizowabana ili kuwavutia wanaume. Kisha mandhari ya klabu maarufu ya *Sabina Joy* yalionyesha sehemu ya nje iliyoko na bango la

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983

klabu ile. Mandhari haya yanasawiri suala la usherati hususan wakati wa usiku. Mandhari haya yanaafikia lengo la kukashifu usherati unaofanyika wakati wa usiku haswa kwa kuuhusisha na dawa za kulevya.

Mandhari haya ya usiku katika video ya wimbo wa kizazi kipya wa *Pombe* wake Rose Muhando yalichangia katika vita dhidi ya mihadarati katika jamii. Mandhari haya yamesawiri athari ya dawa za kulevya kwa mraibu, familia yake na jamii kwa jumla. Hii ni kwa sababu nyingi ya dhuluma kwa waraibu wa dawa za kulevya hufanyika usiku. Hivyo basi, mandhari haya yametumika kupiga vita uraibu wa dawa za kulevya katika jamii kwa waraibu kuepukana na dawa za kulevya hususan wakati wa usiku.

**HITIMISHO**

Makala haya yalihusu mandhari yalivyohusishwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika video za nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Makala haya yalilenga kubainisha jinsi mandhari yalivyotumika katika kupiga vita uraibu wa dawa za kulevya katika video za nyimbo za kizazi kipya. Nyimbo za kizazi kipya zilizolenga suala hili ibuka la dawa za kulevya zilitafitiwa kwa kurejelea mchango wake katika mapambano ya dawa za kulevya mtandaoni.

Matokeo yalionyesha kwamba aina mbalimbali ya mandhari ilibainika katika nyimbo kuhusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni. Mandhari ya nyumbani, barabarani, mjini, mtaani, klabu na mandhari ya wakati yalibainika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mandhari ya klabu na yale ya mjini yakitumika kuonyesha usherati kama athari ya dawa za kulevya. Mandhari ya barabarani yalitumika katika kusawiri maandamano ya wana jamii na mabango dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Mandhari ya klabu pia yalisawiri wizi kama athari mojawapo ya matumizi ya dawa za kulevya. Hatimaye mandhari ya wakati yalitumika kuashiria athari mbalimbali za dawa za kulevya kama vile kutelekeza majukumu na ukosefu wa heshima katika jamii.

Makala haya yalipendekeza kuwa kuna haja ya kuchunguza mandhari kuhusiana na mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kurejelea aina nyinginezo za nyimbo mbali na zile za kizazi kipya. Pili, ni vyema mandhari yatafitiwe katika tanzu nyingine za fasihi pepe kama vile vichekesho, filamu na vipindi vya runinga kwa kurejelea suala la dawa za kulevya.

**MAREJELEO**


Baker, M. (2019). *The Role of Daylight in Narrative Settings: An Analysis*. New York, NY: Academic Press.

Burns, R. B. (2000). *Introduction to Research Methods*. London: SAGE Publishers.

Foley, J.M. (2002). *How to Read an Oral Poem*. Urbana: University of Illinois Press.

Gitau, P.W., Mutai, J., Kiiyukia, C., & Gitonga, M. (2016). Factors Associated with Non-Adherence to Regulations on Sale of Alcohol-by-alcohol Outlets Operators in Thika Municipality, Kiambu County. *East African Medical Journal*, 93(8), 357-366.

Jones, D., Moodie, C., Purves, R.I., Fitzgerald, N., & Crocket, R. (2022). Alcohol Packaging as a Promotional Tool: A Focus Group Study with Young Adult Drinkers in Scotland. *Journal of Studies on Alcohol and Drugs*, 83(4), 565-573. https://doi.org/10.15288/jsad.2022.83.565

Jwan, O & Ong'ondo, C. (2011). *Qualitative Research: An Introduction to Principles and Techniques.* Eldoret: Moi University Press.

Kombo, D.K & Tromp, D.L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi, Kenya: Paulines Publication Africa.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2983


Kress, G. (2008). Meaning and Learning in a World of Instability and Multiplicity. *Studies in Philosophy and Education*, *27*(4), 253-266.

Kristin, G.E. (2002). *Qualitative Methods in Social Research.* New York: The McGraw-Hill Companies.

Mavisi, R., & Wendo, N. (2022). Usawiri wa Mandhari Kibibliotherapia katika Hadithi Fupi teule za Kiswahili**.** *Eastern Africa Journal of Kiswahili*, 1(1), 33-42. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.137

Mbeere, C.K. (2022). *Usawiri wa Dawa za Kulevya katika Matini teule za Fasihi ya Watoto ya Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Chuka, Chuka, Kenya.

Muia, S.T. (2023). *Mchango wa Mandhari katika Kufanikisha Ujumbe katika Riwaya Rosa Mistika na Maisha Kitendawili* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Machakos, Machakos, Kenya.

Mutisya, C.M. (2021). *Usawiri wa Mandhari katika Embe Tamu (Njogu, 2003), Siku ya Wajinga (Momanyi, 2005) na Njiapanda (Amana, 2008)* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

Nyamemba, R. (2015). *Uchanganuzi Linganishi wa Masuala ya Vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na Waandishi katika Diwani ya Tunu ya Ushairi* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Ogechi, O.N. (2022). *Taratibu za Kuendesha Utafiti na Masuala Mengine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Schechner, R. (1985). *Between Theatre and Anthropology*. Philadelphia: Pennsylvania University Press.

Sikuomba, B., & Bulaya, J. (2023). Matumizi ya Mandhari za Kifasihi Simulizi katika Ujenzi wa Dhamira za Ushairi Andishi: Mifano kutoka Diwani za Muhammed Seif Khatib. *Kioo cha Lugha*, 21(2), 200 - 217. DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i2.2

Stringer, E.T. (2007). *Action Research* (3rd ed.). Thousand Oaks, CA: Sage Publications.

Turner, J.H. (1988). *A Theory of Social Structure*. Stanford: Stanford University Press.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Mulwa Publishers Ltd.

World Drug Report. (2022). *Executive Summary: Policy Interventions.* (No. 1) United Nations Publication


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.